# Ahamasisha unywaji maziwa, ulaji nyama

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewataka Watanzania kujenga utamaduni wa kunywa maziwa yaliyosindikwa na bidhaa zake pamoja na kula nyama bora zilizozalishwa, kuchakatwa na kukaguliwa na wataalamu wa mifugo.

Katibu Mkuu wa Mifugo katika Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Prof. Elisante Ole Gabriel, alitoa wito huo jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani yaliyofanyika Njombe.

"Tujizoeshe na watoto wetu kutumia bidhaa za mazao ya mifugo zilizosindikwa na kuchakatwa ikiwa pamoja na maziwa freshi, mgando, jibini, samli, siagi, na hata maziwa ya unga.

"Bidhaa zote hizi ni bora, salama, zinajenga afya bora na kuongeza kiwango cha ufahamu kwa watoto," alisema.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo, kiongozi huyo alisema hadi mwezi uliopita jumla ya shule 210 zenye wanafunzi 89,922 zimenufaika na mradi wa maziwa shuleni katika mikoa 10.

Alitaja mikoa hiyo kuwa ni Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Dar es Salaam, Iringa, Mbeya, Njombe, Morogoro, Mwanza na Mara.

Alisema lita 12,023,186.83 za maziwa zenye thamani ya takribani Sh bilioni 19.24 zimenywewa katika vipindi tofauti kuanzia mwaka 2006 hadi 2020. "Kwa mwaka 2020/21 programu za unywaji maziwa zinaendelea kutekelezwa katika shule 30 kutoka shule 210 zilizokuwa zikitekeleza mpango huo hapo awali. Mikoa inayotekeleza mpango huu kwa sasa ni Kilimanjaro (Shule 24), Iringa (Shule 2) na Mbeya (Shule 4) na hii ni kwa ushirikiano wa wazazi na wasindikaji," alisema. Alisema kufanyika kwa maadhimisho hayo mkoani humo imekuwa ni chachu ya kuwashawishi wadau wa maziwa, viongozi wa serikali, wa kisiasa na kidini kushirikiana na wazazi kuhakikisha mpango huo unatekelezwa katika shule zote.

"Wizara imejipanga kuhakikisha uzalishaji wa maziwa unaongezeka ikiwa ni pamoja na kuongeza ushirikiano na wadau wa tasnia ya maziwa," alisema.

Prof. Gabriel alisema kutoka mwaka 2015/16 hadi mwaka 2019/20 Tanzania imefanikiwa kuwa na jumla ya viwanda vipya 17 vya kusindika nyama na kufanya kuwa na jumla ya viwanda 99 nchini vya kuchakata maziwa, vyakula vya mifugo na nyama.

Alisema wastani wa kusindika maziwa umeongezeka kutoka lita 167,520 mwaka 2015/2016 hadi lita 203,600 kwa siku katika mwaka 2019/2020.

Prof. Gabriel alisema sekta ya uvuvi inachangia asilimia 30 ya protini inayopatikana na wanyama na inatoa ajira kwa Watanzania takribani milioni 4.5 katika shughuli zinazohusiana na uvuvi. Alisema Tanzania ni nchi ya pili Afrika kwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo ikiwa na ng'ombe milioni 33.4, mbuzi milioni 21.29, kondoo milioni 5.65, kuku milioni 83.28, nguruwe milioni 2.14 na punda 657,389.

Alisema ng'ombe hao katika mwaka wa 2019/20, wameweza kuzalisha lita bilioni 3.01 ambapo lita bilioni 2.1 zimetokana na ng'ombe wa asili na lita bilioni 0.9 zimetokana na ng'ombe wa kisasa. Alisema tani 701,679.1 za nyama ziliweza kuzalishwa katika kipindi cha mwaka 2019/20 ikilinganishwa na tani 690,629 zilizozalishwa mwaka 2018/19.

Scanned with CamScanner